



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



TAARIFA KWA UMMA

KAMPENI YA CHANJO YA MATONE YA POLIO AWAMU YA NNE

Kampeni ya Chanjo ya matone ya polio awamu ya nne itatolewa kwa watoto wote wenye umri wa chini ya **miaka 5 (miezi 0 mpaka miezi 59)** kwa muda wa siku nne kuanzia **tarehe 01- 04 Disemba 2022.**

Takriban watoto **laki moja thelathini na moja mia nane ishirini na nane (131,828)** wanatarajiwa kupatiwa chanjo hii.

Kampeni hii itafanyika katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya serikali na binafsi vinavyopatikana katika Manispaa ya Ilemela, nyumba kwa nyumba na maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile sokoni.

Sambamba na uchanjaji huduma zingine zitatolewa ikiwemo elimu ya chanjo na kuimarisha huduma za chanjo katika vituo vya kutolea chanjo.

Polio ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya polio, ugonjwa huu unasababisha kupooza na hatimaye kifo.

KUMBUKA: Mtoto asiyepata chanjo ni hatari kwa maisha yake na jamii inayomzunguka sababu anaweza kuambukizwa magonjwa na kuambukiza wengine

**Violencea S. Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
30/11/2022**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,

Tovuti: www.ilemelamc.go.tz